TANGA MISSIONS SCHOOL

# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

Fomu hii ina sehemu tatu. Jaza sehemu ya kwanza katika nafasi iliyo wazi. Sehemu ya pili ijazwe katika karatasi ya pembeni (unaweza kuandika kwa Mkono au ichapwe) na sehemu ya tatu, unatakiwa usome kwa taratibu na kwa umakini kisha uweke sahihi yako.

Ambatanisha fomu zilizojazwa na ile ya mchungaji wako na kutuma kwa barua pepe.: **tms-admin@omsmissions.or**g

Au unaweza kutuma kupitia anwani ifuatayo:
**Chuo cha Umisheni Tanga, S.L. P. 20, Tanga.**

Kwa maelezo Zaidi piga simu: **0755195159/0623198495**

# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE
{Sehemu I}

**TAARIFA BINAFSI**

Majina kamili

Tarehe ya Kuzaliwa

Uraia

Namba ya Kitambulisho/ pasipoti

Anwani ya Posta

Namba ya simu

**TAARIFA ZA KIELIMU**

Elimu ya Msingi

Elimu ya Sekondari

Chuo

**TAARIFA ZA KIFAMILIA**

Umeoa/ kuolewa?

Je unaishi na mwenzi wako?

Je mwenzi wako amekubali ujiunge na shule ya TMS?

Una watoto?  Andika majina na umri wao?

Nani atakuwa na watoto kwa kipindi utakachokuwa shuleni?

**UZOEFU WA KAZI/ HUDUMA**

Aina ya Huduma

Nafasi/majukumu/Ngazi

Shirika

Mahali

**HALI YA KIFEDHA**

*Ada ya  shule kwa kipindi cha miezi sita ya mafunzo ni Shilingi Tzs. 500,000. Kiasi hichi kinaweza kulipwa kwa awamu.*

Umeajiriwa/umejiajiri?

ajira gani?

Unaweza lipa ada  mwenyewe?

La sivyo, ni nani atakaye kusaidia?

# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE
{Sehemu II}

**HISTORIA NA WITO WA HUDUMA ULIYOITIWA**

*Andika jibu lao angalau aya moja kwa kila swali kwa karatasi la pembeni*

1. Elezea jinsi ulivyookoka.
2. Kwa nini unataka kujiunga na chuo cha umisheni?
3. Unavipawa gani vya kiroho?
4. Umefanikiwa kwa kiwango gani katika huduma?
5. Je unaamini kuwa una wito wa kuwa Mmisheni? Kama ndiyo, elezea kwa kifupi. Umeitwa kufanya nini? Una wito kuwafikia watu gani?
6. Je, Uko tayari kuacha yote na kufanya kile ambacho umeitiwa baada ya kuhitimu?
7. Kuna chochote unachoweza kueleza kuhusu maisha yako?

# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE
{Sehemu III}

**MAMBO YA KUZINGATIA**

kama mwanafunzi wa TMS tunatarajia ufuate sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Shule haitavumilia yeyote atakayejihusisha na ugomvi, ulevi, na uasherati na uzinzi. Ikiwa wewe ni mwana ndoa unatakiwa uwe mwaminifu katika ndoa yako. Atakayebainika amekwenda kinyume na sheria hizo ataondolewa muda huo huo. Tunashauri wanafunzi wote kutojihusisha na maswala ya kimapenzi katika kipindi wakiwa shuleni.
Katika kipindi cha mafunzo utakuwa unaishi na wengine katika bweni. Kawaida wanafunzi wanne wanashirikiana katika chumba kimoja. Gharama ya malazi itatokana na ada.

Kipindi hichi cha mafunzo katika TMS ni kipindi cha kuzingatia. Kwani ndio wakati ambao Mungu atakuwezesha kwa ajili ya wito ulionao. Maisha yako yatabadilika. Utakuwa na ujasiri na uhakika katika Imani yako. Utahubiri Injili kwa ujasiri na nguvu hata katika mazingira magumu.

Ikiwa utajiunga na TMS, utatakiwa kujua kwamba tunafundisha kufikia wale ambao hawajafikiwa na Injili ambao wengi wao ni Waislamu. Utafundishwa jinsi ya kuwafikishia ujumbe wa kiroho kwa ufanisi. Katika kipindi cha mafunzo mtatumwa kuwafikia katika maeneo yao ambapo unaweza kupata changamoto hatarishi wakati wa kuhubiri. Lazima uwe tayari kukabiliana na hali yoyote itakayojitokeza.

Hesabu gharama !

**WAJIBU WETU KWA WANAFAUNZI**

Ikiwa utajiunga na TMS , ni wajibu wetu kufundisha stadi kazi ya huduma. Walimu wetu ni wenye uzoefu katika huduma. Wanatoka katika maeneo mbalimbali. Kuna manabii, mitume, walimu na wainjilisti. Na watu wa vitendo. Hawatafundisha tu kitu cha kufanya bali watakuonyesha namna ya kufanya. Mkienda nje kuhubiri walimu ndio wataongoza wakihubiria wale ambao hawajafikiwa.

Wakuu wa idara katika TMS wamejitoa kwa uwaminifu mbele za Mungu. Hivyo unapoishi katika dhambi watakukemea. Hatutafumbia macho dhambi. Tutakuombea wewe na hatima ya maisha yako, na kufanya lolote ndani ya uwezo wetu kukusaidia kuyatimiza malengo yako .

Hatuahidi kwamba wanafunzi wote wanaohitimu watakuwa wamisheni kwa ufadhili wa TMS. Ingawa TMS itawafadhili na kutuma baadhi ya Wamisheni, lakini wanafunzi wanahitajika kusaidiwa na makanisa yao ya nyumbani. Hata ikiwa hutatumwa na TMS baada ya kumaliza mafunzo, tutakuombea na kusaidia kupiga hatua nyingine katika wito wako.

**SAHIHI**

Jina ______________________ Tarehe ______________

Sahihi

______________________

# MAONI YA MCHUNGAJI

**MAONI YA MCHUNGAJI**

Jina la mwombaji

*Mwombaji angependa kujiunga na shule ya umisheni ,'Tanga Missions School' kama mwanafunzi. Tunaomba maoni yako na taarifa sahihi kuhusiana na huduma pamoja na ushirika wake, katika kanisa lako.*

1. Unamfahamu Mwombaji kwa kipindi gani
2. Una uhusiano gani na yeye?
3. Ni vipaji vipi vya kiroho umewahi shuhudia/kugundua katika utenda kazi wake?
4. Ni majukumu yapi amewahi shughulika nayo katika kanisa/ huduma? Ufanisi wake ulikuwaje?
5. Elezea mwenendo na tabia yake? Je ni mtu mwadilifu, anayeweza kusimamia fedha? Anaweza kuaminika kuyatekeleza majukumu yake?
6. Je Unaamini kwamba mwombaji ameitwa kuwa mmisheni? Unakubali uamuzi wake wa kujiunga na Tanga Missions School?

UMS PASTORAL
**RECOMMENDATION FORM**

**MAONI YA MCHUNGAJI**

7. Baada ya huyu Mwanafunzi kuhitimu, Je kanisa lina mpango wa kumfadhili na kumtuma kama Mmisheni? Kama ndio,unaweza kutushirikisha.

**SAHIHI**

| | |
|---|---|
| jina | baruapepe |
| cheo | Namba ya simu |
| Sahihi | Jina la Kanisa/Huduma |